Serengeti Teachers' Environmental Program - STEP

Heri Ya Mwaka Mpya

2019

SERENGETI PRESERVATION FOUNDATION

Julius K. Nyerere
Arusha Manifesto 1961

“Kudumisha uhai wa wanyamapori wetu ni suala linalotuhusu sana sisi sote katika bara la Afrika. Viumbe hawa wa porini pamoja na mapori wanamoishi siyo tu kwamba ni muhimu Kama mambo ya kustaajabisha na kuvutia, bali pia kwamba ni sehemu muhimu ya maliasili yetu na ustawi wa maisha yetu katika siku za baadaye.

Kwa kukubali dhamana ya kuhifadhi wanyama wetu tunatoa Tamko la dhati kuwa tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha kuwa wajukuu na watoto wetu wataweza kufaidi utajiri na thamani ya urithi huu.

Kuhifadhi wanyamapori na mapori waishimo kunahitaji utaalamu maalumu, watumishi waliofunzwa pamoja na fedha. Tunatazamia kupata ushirikiano kutoka kwa mataifa mengine katika kutekeleza Jukumu hili muhimu. Kufanikiwa au kushindwa kwa Jukumu hilo kutaathiri siyo tu Bara la Afrika pekee, bali Ulimwengu mzima“

“Napenda kutembelea Serengeti niwaone simba wakiwa wamelala.”

Katika kuendeleza maono ya Rais Nyerere nchini Tanzania, Programu ya STEP inawafundisha wanafunzi uhifadhi wa mazingira ili kuwasaidia wawe mabalozi wa asili katika jamii zao.

“Tunapenda kuona picha zetu na wanyama kwenye Kalenda.”

Lilac-breasted roller

Januari 2019

Jumapili	Jumatatu	Jumanne	Jumatano	Alhamisi	Ijumaa	Jumamosi
		1 Mwaka Mpya	2	3	4	5
6	7	8	9	10	11	12 Siku Ya Mapinduzi Ya Zanzibar
13	14	15	16	17	18	19
20	21	22	23	24	25	26
27	28	29	30	31		

STEP inawapa walimu mtaala wa mazingira kutokana na vigezo vya kisayansi nchini Tanzania kwa kujumuisha zana za ufundishaji madarasani, mafunzo ya utumiaji wa zana hizo na ufuatiliaji katika kuzitembelea shule shiriki kupitia wakufunzi wa mradi.

Februari 2019

Jumapili	Jumatatu	Jumanne	Jumatano	Alhamisi	Ijumaa	Jumamosi
Walimu na wanafunzi wanaoshiriki katika STEP hutembelea katika hifadhi za taifa ili kujifunza kuhusu wanyamapori wa Tanzania na jinsi ya kuwalinda wanyama hao.					1	2
3	4	5	6	7	8	9
10	11	12	13	14	15	16
17	18	19	20	21	22	23
24	25	26	27	28		

Cape buffalo
Nyati

Furaha tukiwa mbugani.

Ardhi yenye nyasi

Milipuko ya volkeno katika volkano za miinuko ya juu miaka milioni 3 iliyopita ilipelea ardhi maeneo hayo kufunikwa na majivu ya volkano yenye madini mengi. Hii ilipelekea ardhi ya uwazi ya Serengeti kuwa sehemu kubwa ya malisho kwa wanyama na kuifanya kuwa sehemu pekee iliyobaki kuwa na idadi kubwa ya wanyama wenye kwato wanaoishi kwa kuhama hama duniani. Nyumbu wameliimarisha eneo hili kwa miaka milioni 1.5.

Uhamaji

Jumla ya Nyumbu milioni 1.3, Pundamilia 200,000 na Swala Tomi 200,000 husafiri kilometa 2,900 kwa mwaka kwa kufuata misimu ya mvua. Pundamilia huongoza safairi hii ya kuhama. Meno yao makali hushambulia sehemu za juu za majani na kusaidia uzalishwaji wa madini katika majani hayo ambayo huchochea ukuaji wa majani mapya na mashina yaliwayo na Nyumbu ambao hufuata nyuma ya Pundamilia. Pundamilia wana uwezo mkubwa wa kukumbuka njia waliyopita na uwezo wao mzuri wa kuona na kusikia huwasaidia kutoa mfumo wa tahadhari mapema mara tu wamuonapo adui.

Nyumbu wana uwezo mkubwa sana wa kunusa, hali hii huwasaidia wanyama hawa katika kundi kugundua sehemu yenye maji. Nyumbu huzaa na kulea watoto maeneo yenye majani machanga katika udongo wenye madini mengi ya kivolkeno katika uwazi wa Serengeti. Watoto 500,000 huzaliwa ndani ya wiki 2-3, hii huwasaidia wanyama hawa kuendelea na uhamaji wao hata kama wengine wataliwa na maadui.

Machi 2019

Jumapili	Jumatatu	Jumanne	Jumatano	Alhamisi	Ijumaa	Jumamosi
					1	2
3	4	5	6	7	8	9
10	11	12	13	14	15	16
17	18	19	20	21	22	23
24	25	26	27	28	29	30
31						

Wildebeest and Zebra
Nyumbu na Punda milia

Aprili 2019

Jumapili	Jumatatu	Jumanne	Jumatano	Alhamisi	Ijumaa	Jumamosi
	1	2	3	4	5	6
7 Siku Ya Karume	8	9	10	11	12	13
14	15	16	17	18	19 Ijumaa Kuu	20
21 Jumapili Ya Pasaka	22 Jumatatu Ya Pasaka	23	24	25	26 Sikukuu Ya Muungano	27
28	29	30				

Ikolojia ya Serengeti ina aina spishi zaidi ya 60 za wanyama walao majani, zenye idadi kubwa ya wanyama na idadi kubwa ya maadui kuliko sehemu yoyote duniani.

Topi
Nyamera

Thomson gazelle
Swala Tomi

Grant's gazelle
Swala Granti

Hartebeest
Kongoni



Mei 2019

Jumapili	Jumatatu	Jumanne	Jumatano	Alhamisi	Ijumaa	Jumamosi
			1 Sikuu Ya Wafanyakazi	2	3	4
5	6	7	8	9	10	11
12	13	14	15	16	17	18
19	20	21	22	23	24	25
26	27	28	29	30	31	

Chui ndio mnyama jamii ya paka katika paka wakubwa ambae anaongoza kuishi kwa kujitenga, hupendelea maeneo yenye miti na kando kando ya mito mazingiza ambayo wanaweza kuning’iniza vitoweo vyao juu ya miti ili kuvilinda dhidi ya simba na fisi. Takribani chui 1,000 wanapatikana Serengeti.

Juni 2019

Jumapili	Jumatatu	Jumanne	Jumatano	Alhamisi	Ijumaa	Jumamosi
Simba ndio wanyama jamii ya paka na katika paka wakubwa ambao wanaongoza kuishi kiujamaa ambapo kundi linaweza kuwa na wastani wa simba 12-15. Uharibifu wa mazingira, ujangili na mauwaji kutokana na uvamizi wa mifugo ni tishio kubwa sana kwa simba barani Afrika. Serengeti ni moja kati ya maeneo manne pekee yaliyosalia barani Afrika ambapo idadi ya simba inapatikana kwa kuridhisha kwa sasa.						1
2	3	4	5 Eid ul-Fitr	6	7	8
9	10	11	12	13	14	15
16	17	18	19	20	21	22
23	24	25	26	27	28	29
30						

Vitalu vya miti katika shule ya Sekondari Soitsambu na shule ya msingi Ololosokwan ambapo wanafunzi hupanda miti.

We need
Environment for
our survival

Julai 2019

Jumapili	Jumatatu	Jumanne	Jumatano	Alhamisi	Ijumaa	Jumamosi
	1	2	3	4	5	6
7 Siku Kuu Ya Saba Saba	8	9	10	11	12	13
14	15	16	17	18	19	20
21	22	23	24	25	26	27
28	29	30	31			

Duma hukimbia kilometa 110 kwa saa, duma ndio wanyama wanaoongoza kukimbia kwa kasi kuliko wanyama wote waishio ardhini lakini kasi yao kubwa huonekana pale wanapo mkimbiza swala tomi ambapo hubaki kwa takribani dakika 20-30 bila kula baada ya kumkamata. Ili kupunguza kuibiwa kwa vitoweo vyao dhidi ya maadui wengine, duma huwinda majira ya mchana wakati ambao changamoto dhidi ya maadui wengine inakuwa ni ndogo. Duma ni wanyama walio hatarini zaidi kutoweka duniani, hukumbwa na matatizo kama uharibifu wa mazingira na kuzaliana kwa duma wa familia au ukoo mmoja. Takribani duma 250 wanapatikana katika mazingira ya Serengeti.



Tembo, Tembo wa Afrika ndio mnyama mkubwa zaidi kwa wanyama waishio ardhini duniani, ambae hufikia uzito wa kilogramu 7,000. Huishi kwenye kundi linaloongozwa na jike mkubwa ambae kazi yake siyo tu kulinda kundi dhidi ya tembo kutoka kundi linguine bali pia huliongoza kundi katika kutafuta chakula na maji. Huongoza kundi hilo mpaka pale atakapo kufa na baada ya hapo mtoto wake mkubwa wa kike hurithi uongozi huo. Idadi ya tembo Serengeti imekuwa ikipungua hasa kutokana na mahitaji ya meno ya tembo. Changamoto ya ujangili kwa sasa inatishia maendeleo ya uwepo wa tembo.

Agosti 2019

Jumapili	Jumatatu	Jumanne	Jumatano	Alhamisi	Ijumaa	Jumamosi
				1	2	3
4	5	6	7	8 Sikukuu Ya Nane Nane	9	10
11	12 Eid El Haj	13	14	15	16	17
18	19	20	21	22	23	24
25	26	27	28	29	30	31

Septemba 2019

Jumapili	Jumatatu	Jumanne	Jumatano	Alhamisi	Ijumaa	Jumamosi
1	2	3	4	5	6	7
8	9	10	11	12	13	14
15	16	17	18	19	20	21
22	23	24	25	26	27	28
29	30					

Fisi ni wawindaji bora na wala mizoga wanaoambatana, fisi ni wasagaji muhimu sana ambao huzalisha mabaki ya kalsiam yatumiwayo na viumbe wengine kama kobe. Takribani fisi 7,500 wanapatikana Serengeti. Idadi ya fisi inaongezeka siku hadi siku, hii inawezekana ni kutokana na kupungua kwa kasi kwa idadi ya mbwa mwitu wa Afrika hapo Serengeti.

Ngiri ni wanyama walio tawanyika karibu maeneo yote ya savanna ya Afrika na ndio wanyama jamii ya nguruwe pekee ambao wana uwezo wa kuishi katika maeneo yenye kiwango kidogo cha maji kwa miezi kadhaa. Wana uwezo mkubwa sana wa kuchimba kwa kutumia pua zao pana ili kutafuta chakula jamii ya vitunguu na mizizi yenye virutubisho vingi. Wanaishi kwa makundi ya familia ambayo huundwa na jike na watoto wake na hulala kwenye mashimo majira ya usiku ili kujikinga kutokana na maadui.

Kiboko, ingawa viboko huonekana hawana uwezo wakufanya lolote hasa awapo anakula nchi kavu, ila wana uwezo wa kukimbia kwa kasi ya hadi kilometa 40 kwa saa. Hutumia muda mwingi kupoza miili yao ndani ya maji ambapo ni sehemu muhimu sana katika ikolojia ya mazingira hayo. Mijongeo yao huweza kulainisha sehemu ya chini ya ardhi kwenye maji kitu ambacho huwa ni chanzo cha chakula kwa samaki. Viboko pia huanzisha mapitio ya njia za maji kupitia myanzi na sehemu zenye mimea mingi ambayo hutumiwa na wanyama wengine waishio kwenye maji.

Oktoba 2019

Jumapili	Jumatatu	Jumanne	Jumatano	Alhamisi	Ijumaa	Jumamosi
		1	2	3	4	5
6	7	8	9	10	11	12
13	14 Kumbukumbu Ya Nyerere	15	16	17	18	19
20	21	22	23	24	25	26
27	28	29	30	31		

Tanzania tuna takribani viboko 20,000-30,000. Ujangili na uharibifu wa vyanzo vya maji ni tishio kubwa kwa viboko.

Novemba 2019

Jumapili	Jumatatu	Jumanne	Jumatano	Alhamisi	Ijumaa	Jumamosi
					1	2
3	4	5	6	7	8	9
10 Sikukuu Ya Maulid	11	12	13	14	15	16
17	18	19	20	21	22	23
24	25	26	27	28	29	30

Twiga ndio mnyama mrefu kuliko wanyama wote na dume hufikia kimo cha mita 5.5. Huishi kwenye makundi yalio tawanyika na kundi huweza kuwa na twiga 15. Ulimi mrefu wenye kufikia hadi sentimita 45 unawawezesha twiga kuchagua majani yenye vitamin zaidi katika chakula chao. Serengeti kuna twiga takribani 12,000.



Mchwa ingawa siyo rahisi kuwapiga picha kama tembo na simba, mchwa ni mmoja wa wakazi muhimu katika mfumo wa ikolojia ya Serengeti. Kwa kweli, ujazo wao ndani ya udongo unaweza kuzidi yale ya mamalia wote juu ya ardhi.

Mojawapo ya majukumu muhimu ya mchwa katika Serengeti ni mzunguko wa virutubishi na kuupa hewa udongo. Vichuguu hujengwa na matope kutoka chini ya ardhi ya kina na ulioshikiliwa pamoja na mate ya mchwa. Wana mashimo wima ambayo inaweza kukimbia mita kadhaa katika ardhi na kutoa uingizaji hewa kwa jamii ya mchwa. Mchwa hubaki chini ya ardhi na kujenga vichuguu vya vyakula vyao kutokona miti iliyokauka, mizizi ya nyasi na mimea mingine.

Mashimo ndani vichuguu huwa kama nyumba kwa ajili ya aina mbali mbali ya wanyama, pamoja na nyoka na Nguchiro, wakati vichuguu juu ya ardhi hutumika maficho kwa wanyama wawindao na wanaowindwa. Utotoleshaji ukitokea mchwa wenye mabawa huibuka, ulishaji wa mara nyingi inafuata kama aina ya wanyama wanavyofanya.

Desemba 2019

Jumapili	Jumatatu	Jumanne	Jumatano	Alhamisi	Ijumaa	Jumamosi
1	2	3	4	5	6	7
8	9 Sikukuu Ya Uhuru	10	11	12	13	14
15	16	17	18	19	20	21
22	23	24	25 Sikukuu Ya Noeli	26 Noeli Ya Pili	27	28
29	30	31				

Uhifadhi Endelevu ni ule unaowashirikisha Jamii kama Walinzi wa wanyamapori na mazingira na Jamii tuko tayari.

Jamii na Uhifadhi

- Matangazo wiki nzima kuanzia saa 1:00 jioni mpaka saa 2:00 usiku.
- Kuhusisha jamii za ndani na zile zilizo karibu na mazingira ya Serengeti.
- Pamoja na sehemu za taarifa za uhifadhi na maarifa.



- Wasikilizaji wanahamasishwa kushiriki kwa kuuliza maswali na kutoa maoni.
- Watu wazima wanaalikwa kujadili umuhimu wa dunia kwa maisha na tamaduni za kimasai.

Uhifadhi wa Kesho uno mikononi Mwa vijana waliowezesha na kupewa Ujuzi wa Uhifadhi wa wanyamapori na Mazingira.